# Sheria Ndogo

# Za

# (Ada na Ushuru)

# Za

# Halmashauri Ya Wilaya

# Ya Wanging'ombe

*Tangazo La Serikali Na. 185 La Tarehe* **20/06/2014**

TANGAZO LA SERIKALI NA. 185 la tarehe 20/06/2014

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE (ADA NA USHURU) ZA MWAKA 2014

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe za Mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe .

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo;

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au Wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Boliti"maana yake ni miti yote ya ujenzi yenye kipenyo isiyozidi sentimeta kumi na tano.

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"Gulio"maana yake ni sehemu au eneo ambalo limetengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao ya kilimo na mifugo.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe .

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

"Kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya abiria.

''Mbao laini''maana yake ni pamoja na mbao zitokanazo na miti jamii ya misingano mfano, mipaini na mibani mivinje.

''Mbao ngumu''maana yake ni mbao zinazotokana na miti ya asili pamoja na ya kigeni isiyo misindano mfano mikaratusi, milingoti, mitiki msaji na migrevelea.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

"Madini ya Ujenzi" maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Maegesho" Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.

"Soko" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.

"Mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe pamoja na Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Ushuru wa Madini ya Ujenzi" maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Madini ya ujenzi katika maeneo yaliyoruhusiwa tu.

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

Ada na Ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru wa bidhaa, Vibali, na Leseni zitolewazo kama zilivyoorodheshwa kwenye jedwali la sheria Ndogo hizi,

(2) Halmashauri itatenga maeneo ya maalumu kwa ajili ya huduma za Masoko, Gulio, Minada na Machimbo ya Madini.

(3) Ada na Ushuru utatozwa kuanzia Saa Kumi na Mbili asubuhi mpaka Saa Kumi na Mbili jioni, na utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(4) Ada na Ushuru utakaotozwa na Halmashauri utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa Kumi na Mbili Kamili asubuhi mpaka saa Kumi na Mbili jioni.

6.-(1) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmasahuri/wakala na mlipa Ada na ushuru.

(2) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Uteuzi na wajibu wa Wakala

7.-(1) Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa;-

(a) kukusanya Ada na Ushuru kwa kiwango kilichoainishwa na Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa;

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) kuweka dhamana ya kusanyo la Mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba;

(d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba;

(e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala Kwa kila mwezi;

(f) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

Makosa

8.-(1) Wakala yeyote ambaye;-

(a) Atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b). Atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Mtu yeyote ambaye;

(a) Atashindwa, atadharau, au atakaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lo lote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatumza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atashindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri;

(f) Atachimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyoidhinishwa na Halmashauri.

(g) Atachimba shimo kubwa chini ya ardhi kwa ajili ya madini ya ujenzi na kuliacha bila kupanda miti au mimea mara baada ya madini hayo kuisha.

(h) atamzuia Afisa Muidhiwa kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

9. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Chini ya Kifungu cha 4 (1)*

1. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

Ada ya maombi ya kukodi au kutumia jengo au kibanda

| *Na.* | *Huduma* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Jengo/nyumba | 100,000/= kwa mwaka |
| 2. | Kibanda kidogo | 15,000/= kwa mwaka |
| 3. | Kibanda kikubwa | 40,000/= kwa mwaka |
| 4. | Kioski | 15,000/= kwa mwaka |
| 5. | Meza | 10,000/= kwa mwaka |

2. ADA NA USHURU WA MAZAO

| *Na.* | *Zao* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 5% ya Bei ya kununulia |
| 2. | Mchele | 5% ya Bei ya kununulia |
| 3. | Maharage | 5% ya bei ya kununulia |
| 4. | Viazi mviringo | 5% ya Bei ya kununulia |
| 5. | Ngano | 5% ya Bei ya kununulia |
| 6. | Alizeti | 5% ya Bei ya kununulia |
| 7. | Matunda | 5% ya Bei ya kununulia |
| 8. | Miwa | 5% ya Bei ya kununulia |
| 9. | Nyanya | 5% ya Bei ya kununulia |
| 10. | Karanga | 5% ya Bei ya kununulia |
| 11. | Mpunga | 5% ya Bei ya kununulia |
| 12. | Kahawa | 5% ya Bei ya kununulia |
| 13. | Pareto iliyokaushwa | 5% ya Bei ya kununulia |
| 14. | Chai-Green tea | Tsh. 12 kwa kilo |
| 15. | Maua | Tsh. 15 kwa kilo |

3. ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA NA MNADA

| *Na.* | *Ada/Ushuru* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya Machinjio kwa kila ng'ombe atakayechinjwa | 3,000/= kila mmoja |
| 2. | Ada ya Machinjio kwa kila Kondoo, Mbuzi na Nguruwe atakayechinjwa | 500/= kila mmoja |
| 3. | Ukaguzi wa nyama | 1,500/= |
| 4. | Ushuru wa Bucha la Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, na Samaki | 500/= kwa siku |
| 5. | Ushuru wa Ng'ombe anayepelekwa mnadani | 5,000/= kwa siku |
| 6. | Ushuru wa Mbuzi/kondoo anayepelekwa mnadani | 3,000/ Kwa siku |

I. ADA NA USHURU WA BIDHAA ZA GULIONI NA SOKONI

| *Na.* | *Bidhaa/huduma* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| | Mauzo ya bidhaa za viwandani (yasiyo ya vyakula) | 1000/= kwa siku |
| | Mauzo ya bidhaa za viwandani (vyakula) na bidhaa nyingine | 500/= kwa siku |
| | Ushuru wa Meza sokoni | 200/= Kwa siku |
| | Ushuru wa Kibanda sokoni | 200/= Kwa siku |

4. Majengo mengine 15,000/

6. ADA YA UKAGUZI NA IDHINI YA UJENZI

| *Na* | *Aina ya Jengo* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Minara ya simu | 200,000/ kwa kibali |
| 2. | Ghorofa | 250,000/ kwa kibali |
| 3. | Nyumba ya biashara (Guest house,Maduka) | 50,000/ kwa kibali |
| 4. | Kituo cha mafuta | 200,000/= kwa kibali |
| 5. | Nyumba ya makazi | 20,000/= kwa kibali |
| 6. | Nyumba ya makazi na biashara | 30,000/= kwa kibali |
| 7. | Ofisi binafsi, mashule binafsi na hospitali binafsi | 100,000/= kwa kibali |
| 8. | Maghala na bohari | 100,000/= kwa kibali |

7. USHURU WA MAGULIO

MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA MASOKO NA MAGULIO

| Na | TARAFA | KATA | MAGULIO | KIJIJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mdandu | Mdandu | 1.Itambo<br>2.Itulahumba<br>3.Mungate<br>4.Sakalenga<br>5.Mdandu<br>6.Itowa<br>7.Ihanja<br>8.Isindagosi | 1.Itambo<br>2.Itulahumba<br>3.Mungate<br>4.Sakalenga<br>5.Mdandu<br>6.Itowa<br>7.Ihanja<br>8.Isindagosi |
| 2 | | Usuka | 1.Usuka<br>2.Matowo<br>3.Ikwega<br>4.Lugoda<br>5.Iteni | 1.Usuka<br>2.Matowo<br>3.Ikwega<br>4.Lugoda<br>5.Iteni |
| 3 | | Igwachanya | 1.Palangawanu<br>2.Kanani<br>3.Chalowe<br>4.Dulamu<br>5.Idindilimunyo<br>6.Mtapa<br>7.Igwachanya | 1.Palangawanu<br>2.Kanani<br>3.Chalowe<br>4.Dulamu<br>5.Idindilimunyo<br>6.Mtapa<br>7.Igwachanya |
| 4 | | Igima | 1.Igima<br>2.Mlevela<br>3.Lulanzi<br>4.Lusisi<br>5.Mhaji | 1.Igima<br>2.Mlevela<br>3.Lulanzi<br>4.Lusisi<br>5.Mhaji |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | 6.Nyumbanitu<br>7.Mawindi | 6.Nyumbanitu<br>7.Mawindi |
| 5 | | Wangama | 1.Imalilo<br>2.Wangama | 1.Imalilo<br>2.Wangama<br>3.Usalule |
| | | Makonga | 1.Makoga<br>2.Utelewe<br>3.Ng'anda<br>4.Uhekule<br>5.Samaria<br>6.Idunda | 1.Makoga<br>2.Utelewe<br>3.Ng'anda<br>4.Uhekule<br>5.Samaria<br>6.Idunda |
| | | Imalinyi | 1.Imalinyi<br>2.Igodivaha<br>3.Masaulwa<br>4.Kinenulo<br>5.Ilulu | 1.Imalinyi<br>2.Igodivaha<br>3.Masaulwa<br>4.Kinenulo<br>5.Ilulu |
| | | Kidugala | 1.Kidugala<br>2.Masilu<br>3.Masage<br>4.Gonelamafuta | 1.Kidugala<br>2.Masilu<br>3.Masage<br>4.Gonelamafuta |
| | | Ulembwe | 1.Usalule<br>2.Ulembwe<br>3.Igagala | 1.Usalule<br>2.Ulembwe<br>3.Igagala |
| | | Igosi | 1.Ujindile<br>2.Mdasi<br>3.Igosi<br>4.Ivigo | 1.Ujindile<br>2.Mdasi<br>3.Igosi<br>4.Ivigo |
| | | Kipengere | 1.Mwilamba<br>2.Mafinga<br>3.Moronga<br>4.Kipengere<br>5.Ing'enyango | 1.Mwilamba<br>2.Mafinga<br>3.Moronga<br>4.Kipengere<br>5.Ing'enyango |
| | Wanging'ombe | Saja | 1.Saja<br>2.Isimike<br>3.Uhenga<br>4.Itengelo<br>5.Igoma<br>6.Ikulimambo<br>7.Idenyimembe<br>8.Igenge | 1.Saja<br>2.Isimike<br>3.Uhenga<br>4.Itengelo<br>5.Igoma<br>6.Ikulimambo<br>7.Idenyimembe<br>8.Igenge |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanging'ombe | 1.Ufwala<br>2.Utiga<br>3.Mng'elenge<br>4.Mayale<br>5.Wanging'ombe<br>6.Katenge<br>7.Itandula | 1.Ufwala<br>2.Utiga<br>3.Mng'elenge<br>4.Mayale<br>5.Wanging'ombe<br>6.Katenge<br>7.Itandula |
| | | Kijombe | 1.Kijombe<br>2.Lyamluki<br>3.Lyadebwe<br>4.Ukomola<br>5.Ikwavila | 1.Kijombe<br>2.Lyamluki<br>3.Lyadebwe<br>4.Ukomola<br>5.Ikwavila |
| | | Luduga | 1.Hanjawanu<br>2.Iyayi<br>3.Mambegu<br>4.Luduga<br>5.Korintho<br>6.Malangali<br>7.Igando<br>8.Mpanga | 1.Hanjawanu<br>2.Iyayi<br>3.Mambegu<br>4.Luduga<br>5.Korintho<br>6.Malangali<br>7.Igando<br>8.Mpanga |
| | | Ilembula | 1.Udonja<br>2.Knamalenga<br>3.Mpululu<br>4.Igula<br>5.Banawanu<br>6.Igelegedza<br>7.Ilembula<br>8.Iponda<br>9.Ujange<br>10.Kasagala | 1.Udonja<br>2.Knamalenga<br>3.Mpululu<br>4. Igula<br>5.Banawanu<br>6.Igelegedza<br>7.Ilembula<br>8.Iponda<br>9.Ujange<br>10.Kasagala |

JEDWALI LA PILI
HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA
*(Chini ya kifungu cha 11)*

Mimi ...................... nakiri mbele ya ............ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, kwamba mnamo tarehe ...... ya Mwezi ....... Mwaka ...... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ...... cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe (Ada na Ushuru) za Mwaka 2014.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe............ ya Mwezi........... Mwaka .....................
*Jina*.................................... *Saini*.......................................

Mbele ya :

Jina: ..................................................
Cheo: ..................................................
Saini: ..................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe ilibandikwa kwenye Kanuni za Kudumu hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 28 - 29 mwezi 01 m waka, 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:-

LUCY L. MSOFFE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe*

ANTHON E. MAHWATA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Songea*

NAKUBALI

Dodoma,
11 Aprili, 2014

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB),
*Waziri Mkuu*